Namba ya Mtahiniwa: ..............................

# BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA

## MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU

## KIDATO CHA PILI

## KISWAHILI

**021**

**MUDA: Saa 2:30** **Ijumaa, 31 Julai 2026 Mchana**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi (10).
2. Jibu maswali yote.
3. Sehemu A ina alama **kumi na tano (15),** sehemu B ina alama **sabini (70)** na sehemu C ina alama **kumi na tano (15).**
4. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi.
5. Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizopewa.
6. Vifaa vya maswasiliano na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
7. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

Shulelibrary.com

| KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **SAINI YA MTAHINI** |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| **JUMLA** | | |
| **SAINI YA MKAGUZI** | | |

Namba ya Mtahiniwa: .............................

## SEHEMU A (Alama 15)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Katika kipengele (i) – (x) chagua jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika jedwali ulilopewa hapo chini.

(i) Mzee Mitomingi alisikika akisema “Mbuzi zangu wamepotea.” Ukiwa kama mjuzi wa sarufi ya Kiswahili ni kosa gani mzee huyo alilifanya?

A. Kosa la kisintaksia
B. Kosa la kimatamshi
C. Kosa la kiupatanisho
D. Kosa la kimantiki

(ii) Wanafunzi wa kidato cha kwanza walipewa kazi ya kuandika barua kwa wazazi wao ili waje kuwatembelea siku ya Jumamosi. Ni kipengele kipi kinafuata katika barua zao baada ya anuani ya mwandishi?

A. Salamu
B. Tarehe
C. Jina la mwandishi
D. Kiini cha barua

(iii) Bahati na Sikujua walisoma kitabu kinachotoa fasili ya ufahamu. Fasili sahihi ilipatikana humo. Ipi kati ya sentensi zifuatazo huhusika katika jibu lililosomwa na Bahati pamoja na Sikujua?

A. Kuona, kusikiliza na kutafakari
B. Kusoma, kusikiliza na kuona
C. Kuona, kusikiliza na kusoma
D. Kusoma, kufikiri na kuelewa

(iv) Watanzania wana utamaduni wao madhubuti ikiwemo lugha ya Kiswahili. Je, vipengele vipi vinahusiana nao?

A. Salamu, mavazi na vyakula
B. Vyakula, kilimo na mavazi
C. Nyimbo, unasibu na mavazi
D. Mavazi, unasibu na vyakula

(v) Matumizi ya ishara katika mazungumzo hutofautiana. Ipi kati ya sababu zifuatazo huleta tofauti hizo?

A. Elimu
B. Umri
C. Utamaduni
D. Mada

Shulelibrary.com

(vi) Kamusi ya Kiswahili imepangwa katika mpangilio ulio sahihi na si kiholela. Je, katika seti zifuatazo, seti ipi ina mpangilio kama huo?

A. Zogo, kisu, shule na dhambi
B. Dhambi, shule, kisu na zogo
C. Zogo, kisu, dhambi na shule
D. Dhambi, kisu, shule na zogo

(vii) Kama ilivyo kwa lugha nyingine, pia vitenzi vya Kiswahili vina viambishi awali na viambishi tamati. Vibaini viambishi awali katika kitenzi "**anayeimba**."

A. a- na – ye-
B. a**,** na, ye
C. a**,** -ye, -i
D. a – na – im

(viii) "Pahali alipopita pana nyoka wengi sana." Sentensi hii inaingia katika ngeli ipi ya nomino?

A. YU/A – WA
B. U – I
C. PA-MU-KU
D. LI – YA

(ix) Kusoma kwa ufahamu na udadisi ni jambo linalobainika kwa vitendo mbalimbali. Ipi kati ya seti zifuatazo huwakilisha aina hiyo ya usomaji?

A. Kusoma kwa kubaini hoja zote zilizomo ndani ya habari
B. Kusoma kwa kubaini Mawazo makuu na kuuliza maswali
C. Kusoma kwa kuzingatia alama za uandishi na sauti kubwa
D. Kusoma kwa kuzingatia lafudhi na kiimbo

(x) Ufupishaji wa habari baada ya kusikiliza mazungumzo ya mdomo una taratibu na kanuni zake zinazopaswa kuzingatiwa. Ipi kati ya sentensi zifuatazo hutaja kanuni hiyo?

A. Kuzingatia alama za uandishi
B. Kuzingatia kiimbo na lafudhi yake
C. Kuzingatia sauti ya mzungumzaji
D. Kuzingatia wazo kuu

**MAJIBU:**

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

Shulelibrary.com

2. Oanisha ngeli za Nomino zilizopo katika orodha A na viambishi ya urejeshi vilivyopo katika orodha B, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika jedwali hapo chini.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| (i) LI – YA | A. CHO-VYO |
| (ii) KI – VI | B. YO – ZO |
| (iii) YU/A – WA | C. ZO – YO |
| (iv) I – ZI | D. O – YO |
| (v) U – YA | E. LO – YO |
| | F. O – ZO |
| | G. YE – O |

**MAJIBU:**

| **ORODHA A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **ORODHA B** | | | | | |

Shulelibrary.com

**SEHEMU B (Alama 70)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

3. Mzungumzaji wa lugha huathiriwa na mambo mbalimbali ili kufikia umahiri wa mazungumzo yake. Kwa hoja tano (5) eleza mambo hayo:

(i) ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(ii) ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(iii) ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(iv) ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(v) ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

4. Azizi ni msomaji wa kazi mbalimbali za Kiswahili lakini anashindwa kusoma matini kwa ufasaha. Kama rafiki yake wa karibu, msaidie kubainisha mambo matano (5) ya kuzingatia ili aweze kutatua tatizo hilo.
   (a) ______________________________
   (b) ______________________________
   (c) ______________________________
   (d) ______________________________
   (e) ______________________________

5. Mzee Matale hupenda kutumia lugha ya mazungumzo kutokana na kujua sifa za lugha hiyo. Ukiwa mjuzi wa lugha hiyo bainisha sifa zake kwa hoja tano.
   (i) ______________________________
   ______________________________
   (ii) ______________________________
   ______________________________
   (iii) ______________________________
   ______________________________
   (iv) ______________________________
   ______________________________
   (v) ______________________________
   ______________________________

Shulelibrary.com

6. Mwalimu wenu wa Kiswahili aliwafundisha kuhusu vipashio vya kimuundo na kugusia dhana ya kirai na aina zake.
   (a) Fafanua maana yake
   ______________________________
   ______________________________
   (b) Bainisha aina nne za kipashio hicho
   (i) ______________________________
   (ii) ______________________________
   (iii) ______________________________
   (iv) ______________________________

7. Kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo huhusisha istilahi mbalimbali. Kwa ufupi eleza maana ya istilahi hizo.
   (i) Lugha ya mazungumzo
   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________

(ii) Mkazo

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

(iii)Kiimbo

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

(iv)Lafudhi

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

8. Soma wimbo ufuataao kisha jibu maswali yanayofuata.

Acha nibaki na raha zangu,
Kwa nini nisifurahi?
Kuzaliwa Tanzania, kwa baba na mama – ni kwetu!
Ni kisiwa cha amani, moyo hautetemeki – hakika,
Pita huku, nenda kule, wasiwasi haupati – ni uhuru,
Kote wendako nyumbani, iwe hata zaramoni – umefika.

<u>Kiitikio</u>
Nihame niende wapi?
Nimefika, siondoki.
Acha nipatunze kwetu.
Hatua tumezipiga maishani
Huoni miundo mbinu? Imejaa

(a) Kipi kinaweza kuwa kichwa cha wimbo uliosoma?

______________________________________________

(b) Mwandishi wa wimbo huu amezaliwa nchi gani?

______________________________________________

(c) Bainisha sifa tatu (3) zinazopatikana katika nchi ya mwandishi.

(i) ______________________________________________

(ii) ______________________________________________

(iii) ______________________________________________

Shulelibrary.com

9. Baada ya kipindi kuisha, mwalimu Zubeda aliwapa kazi wanafunzi wake kutaja kwa mifano aina tano (5) za rejesta. Ukiwa miongoni mwa wanafunzi waliohudhuria kipindi, onesha unavyoweza kutekeleza jukumu hilo.
   (a) Aina : ____________________
   Mfano: ____________________
   (b) Aina : ____________________
   Mfano: ____________________
   (c) Aina : ____________________
   Mfano: ____________________
   (d) Aina: ____________________
   Mfano: ____________________
   (e) Aina: ____________________
   Mfano: ____________________

**SEHEMU B (Alama 15)**

Jibu swali la kumi (10) katika sehemu hii

10. Kumbukumbu za mikutano ni kitu cha muhimu katika kikao ili kutekeleza mipango kazi. Ukiwa kama Katibu wa serikali ya wanafunzi katika shule ya sekondari Songambele, andika kumbukumbu hiyo kwa ajenda tano.

Shulelibrary.com

Namba ya Mtahiniwa: ..............................

***Wabillah Tawfiiq***

Shulelibrary.com